

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

Upimaji wa Haraka wa Antijeni wa COVID-19

Upimaji wa haraka unatofautiana vipi na upimaji wa kawaida wa PCR?

Ingawa matokeo mengi ya upimaji wa PCR huchukua siku chache baina ya wakati sampuli inakusanywa na mtu kuarifiwa, upimaji wa haraka ni zana inayofaa, inabebeka kwa urahisi na ya bei nafuu ya kugundua maambukizi ya virusi vya korona. Watu wanaweza kupima na kupata matokeo ya vipimo ndani ya dakika 15, hivyo basi kuwaruhusu watu walioambukizwa na virusi kujitenga kwa haraka zaidi.

Je, vipimo vya haraka ni sahihi kwa kiwango gani?

Vipimo vya haraka havionyeshi mbadiliko yote na vina kiwango cha juu cha matokeo hasi yasiyothibitishwa na kwa hivyo unaweza kupata matokeo hasi, lakini bado una virusi. Hata kama vipimo vitakuwa hasi, unapaswa kuendelea kuchukua hatua za kujikinga na COVID-19, ikijumuisha kuvaa barakoa na kuzingatia umbali baina yako na wengine. Kupata matokeo chanya yasiyothibitishwa (ambapo matokeo ni chanya, lakini huna virusi) haiwezekani. Vipimo vya PCR ambavyo hufanywa katika maabara vingali kiwango murua cha kupima COVID-19 na ni sahihi sana.

Ni lini ambapo vipimo vya antigen ni sahihi zaidi?

Vipimo vya haraka vya antijeni huwa na matokeo bora zaidi mtu anapokuwa na dalili na kupimwa katika hatua za awali za kuambukizwa na SARS-CoV-2 wakati wingi wa virusi kwa ujumla ni wa juu zaidi. Pia vinaweza kuwa vya kuarifu katika hali za uchunguzi ambapo mtu ana mfiduo unaojulikana wa kisa kilichothibitishwa cha COVID-19.

Mchakato wa upimaji ni upi?

Vipimo vinafanywa kupitia kwa sampuli ya pua katika sehemu ya chini ya pua. Washiriki watasugua pua zao wenyewe chini ya uangalizi katika vituo vya upimaji. Taarifa zaidi kwa watu amao wanapimwa inapatika [kwenye tovuti](#).

- **Je, nikipatikana na Virus?**

Jitenge nyumbani mara moja. Zuru health.nd.gov/covidpositive kwa taarifa zaidi na mchunguzi atawasiliana nawe ndani ya saa 24.

- **Je, nikiwa na vipimo hasi, lakini bado nina dalili?**
Watu wanaopata vipimo hasi, lakini bado wana dalili wanapaswa kupata kipimo cha PCR. Zuru health.nd.gov/testnd kupata eneo lililo kaibu nawe.
- **Je, nikiwa sina Virusi?**
Watu wanapaswa kufuatilia iwapo kutakuwa na dalili. Kupima COVID-19 si kabadala cha hatua za kimsingi za kuzuia kuenea kwa COVID-19, ikijumuisha kudumisha umbali baina yako na watu wengine, kuvaa barakoa, kunawa mikono, kusafisha sehemu zinazoguswa mara kwa mara na kuepuka nafasi za ndani zenye msongamano wa watu.

Je, ninapaswa kupimwa ikiwa hapo awali nilipimwa na kupatikana kuwa COVID-19?

Watu ambao wamepatikana kuwa na COVID-19 ndani ya siku 90 zilizopita hawafai kupimwa tena.

Je, nitasubiri matokeo kwa muda gani, na ninayapata vipi?

Matokeo kwa kawaida yatapatikana kwenye kituo ndani ya dakika 15.

Je, chanjo ya COVID-19 inaweza kukufanya uwe na vipimo chanya vya COVID-19?

La. Vipimo vya virusi vya COVID-19 havitaonyesha matokeo chanya baada ya kupokea chanjo ya COVID-19.